

MTAZAMO WA DINI YA KIISLAM KUHUSU CHANJO

MAANA YA CHANJO :

Chanjo ni dawa anayopewa binadamu au mnyama kwa kutumia sindano au vidonge au njia nyengene yoyote inayokubalika kisheria kwa ajilia ya kumkinga kutokana maradhi ya mripuko au maradhi mengine yanayokhofiwa kutokea baadae.

MTIZAMO WA UISLAM KUHUSU CHANJO :

Katika mambo ambayo uislamu umeyahimiza na kuyatilia mkazo ni suala la kulinda nafsi ya binadamu isidhurike , mpaka ikaruhusu baadhi ya ibada zake za faradhi zisifanyika katika utaratibu wake katika mazingira Fulani kwa kuhofia kudhurika nafsi ya binadamu , kama vile kufunga kwa msafiri , kuswali kwa tayammamu badala ya kutia udhu kwa msafiri mwenye maji kidogo kwa kuhofia kufa kwa kiu , hii yote ni kwa ajili ya kuilinda nafsi ya mwanadamu isidhurike . kwahivyo ikiwa chanjo itathibitika kua kweli inaweza kumkinga mwanadamu na maradhi na haina madhara basi uislamu utaikubali chanjo hiyo na ikikosa moja kati ya masharti hayo mawili uislamu haitoikubali .

DALILI :

ٹ ڈ چ ژ چ

Amesem Allah Mtukufu : *“Na chukueni tahadhari zenu.”*

Maana ya kuchukua tahadhari : Ni kuchukua khatua za kujikinga kutokana na khatari ambayo inakhofiwa kutokea baadae . sawa sawa khatari hiyo iwe ni maradhai au jambo jengine , na chanjo ni khatua ambayo anaichukua binadamu kwa ajili ya kujikinga na maradhi ambayo anakhofia kumpata baadae .

ورد عن رسول الله صلى الله عليه وسلم أنه قال : " من تصبح بسبع تمرات عجوة

لم يضره في ذلك اليوم سحر "

Imepokelewa kutoka kwa Mtume (S.W.A) kua yeye amesema : *“Mwenye kula tende saba ain ya ajwa , hatodhurika siku hiyo kutokana na uchawi”*

Hii ni dalili ya kua kuna baadhi ya vitu ni kinga ya maradhi na mambo mengine mabaya ambayo yanaweza kumpata mwanadamu baadae, Kwahivyo hadithi hii inatujulisha , kula kokwa saba za tende aina ya ajwa ni kinga kutokana na uchawi kam inavyo tujuulisha kua kufanya chanjo kwa ajili kujikinga kutokana na maradhi ambayo yanakhofiwa kutokea badae hamna tatizo sababu mambo yote mawili (kula tende saba na kufanya chanjo) lengo lake ni moja, kujikinga.

وورد عن النبي صلى الله عليه وسلم أيضا أنه قال : 'إذا وقع الذباب في إناء أحدكم فليغمسه كله ثم ليطرحه فإن في أحد جناحيه الداء وفي الآخر شفاء'،

Pia imepokewa kutoka kwa Mtume (S.W.A) hakika yake amesema : “Pindi atakapoingia inzi katika kinywaji cha mmoja wenu basi amzamishe kisha amtote kwani hakika katika moja ya mbawa zake lina maradhi na jengine lina dawa .“

Pia hadithi hii inatilia mkazo umuhimu wa kuchukua tahadhari na kujikinga kutokana na maradhi . Kumzamisha inzi kabla ya kumtoa ni tahadhari na ni kinga ya maradhi ambayo yanakhofiwa kumpata muhusika endapo hatomzamisha , kama vile chanjo ni kinga ya maradhi ambayo yanakhofiwa .

WATU WA MWANZO KUVUMBUA CHANJO

Watu wa mwanzo kuvumbua chanjo ni waislam katika utawala wa Othmaania katiaka mji wa Istambuul mwaka 1724 na waliitumia kwa kuwachanja watoto wao kutokana na maradhi ya _____ baada ya miaka hamsini ndio utaalumu huu ukafika Ulaya kupitia mke wa balozi wa Uingereza nchini Uturuki alieuchukua utaalumu huo na kuupeleka Ulaya .

JE KUFANYA CHANJO NI KWENDA KINYUME NA AKIDA YA KIISLAMU?

Chanjo ni aina ya tiba , na tiba ni halali katika uisbamu bali umehimiza watu kufanya tiba, kwahivyo kufanya chanjo sio kwenda kinyume na akida ya kiislamu na wala haipinagni na suala la kumtegemea Allah sababu hata unapotumia dawa kufanya chanjo unakua unamtegemea Allah aiwafikishe ile dawa yako au chanjo ili iweze kukusaidia .

JE INAFAA KUTUMIA CHANJO ILIOCHANGANYWA NA NAJISI ?

Amesema Imamu Nawawy katika Sherh Muslim : “ Ama kufanya dawa kwa vitu vilovyokua haramu ni haramu , na ama kufanya dawa kwa vitu vinavyochukiza basi kuacha ni bora “ na chanjo ni katiaka dawa kwahivyo ikiwa imetengenezwa kutokana na vitu vya haramu itakua ni haramu na ikiwa imetengenezwa na vitu vinavyochukiza kuacha kutumia ni bora.

Ama baadhi ya wanadhuoni wa zama zetu wako waliosema kua ikiwa itakua hamna chanjo nyengine na kwamba ikiwa hukutumia chanjo hiyo utadhurika basi unaweza kutumia kwa dharura. Na wengine wakasema : ikiwa hiyo najisi iliyochanganywa haiwezekani kutenganishwa, hina tatizo inafaa kutumia .